ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53.Mhe. Asha Bakari Makame	Uteuzi wa Rais.
54. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
55.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
58.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
59.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
60.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
61Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
62.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
63.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
64. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
65.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
66.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

68.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
69.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
70. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
71.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
72.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
73.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
74.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
75.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
76.Mhe. Saleh Ramadhan Feruz	Uteuzi wa Rais.
77.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
78..Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
79.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
80.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 15 Julai, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Thuwaybah Edington Kissasi) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Misamaha na Nafuu ya Kodi iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2009/2010. Pia Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni yake kuhusiana na masuala ya Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima kubwa naomba sasa kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nne na Arubaini na Nne Mia Sita na Thalathini na Nane Milioni Mia Mbili na Sita Elfu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni,

2010/2011 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa waliyotuwezesha sisi Wizara ya Fedha kwanza katika matayarisho ya Bajeti ya Serikali ambayo tuliipitisha awali, halafu pia mashirikiano makubwa katika kuchangia bajeti zote za wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na jana hatimaye kumalizia bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mashirikiano makubwa na maelekezo yenu na maagizo yenu kama nilivyosema jana tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Kwa hiyo, leo ni kama ada yetu tunawasilisha mswada huu kama ni ada ili tupate idhini yenu ya kuweza kuutumia.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu una vifungu vipatavyo vinane. Kifungu cha kwanza kinazungumzia Jina Fupi. Kifungu cha pili kinazungumzia Utoaji wa Shilingi Bilioni Mia Nne na Arubaini na Nne Mia Sita na Thalathini na Nane Milioni Mia Mbili na Sita Elfu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha tatu kinazungumzia Makisio ya Fedha Zilizokubalika. Kifungu cha nne chenye vifungu vidogo vinne vile vile kinazungumzia Uwezo wa Waziri wa Kukopa. Kifungu cha tano chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia Uwezo wa Waziri wa Maombi ya Ziada.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha sita kinazungumzia Marejesho ya Mkopo na Riba. Kifungu cha saba kinazungumzia Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha mwisho kinazungumzia Kukubaliwa kwa Fedha Zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, mswada ni mfupi na kama nilivyosema ni ada. Kwa hiyo, naomba kwa idhini yako na Waheshimiwa Wajumbe kuweza kuujadili na hatimaye kuupitisha mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ali Suleiman Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana kwenye Baraza lako tukufu kwa ajili ya kujadili mambo yenye manufaa kwa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kwanza ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, kwa niaba ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika zoezi la kupitia Bajeti za Wizara za Serikali wakiwa Wenyeviti katika Kamati zao. Vile vile, napenda kuwashukuru kwa ushirikiano wao mzuri waliouonesha wakati wa kazi za Kamati yetu kwa jumla katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii, iliyodumu kwa kipindi cha takriban miaka miwili na nusu, tangu ilipoundwa mwaka 2008; uhai ambao utafikia ukomo baada ya kuvunjwa kwa Baraza hili la Saba. Kamati hii imeundwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omari Kheri - Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji - Mjumbe
4. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu - Mjumbe
5. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mjumbe
6. Mhe. Najma Khalfan Juma - Mjumbe Mualikwa

Kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 Ndugu Mdungi Makame Mdungi na Ndugu Nasra Awadh Salmin walikuwa Makatibu wa Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kubainisha Wajumbe wa Kamati hii, sasa naomba uniruhusu kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, kwa jinsi alivyosimamia zoezi zima la uwasilishaji wa Bajeti ya Serikali ambayo ilimalizika jana jioni, kwa kupitishwa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa mnasaba huo huo, napenda kuwapongeza Watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi, hasa Idara ya Ukuzaji Uchumi na Bajeti kwa kufanyakazi bila kuchoka katika kipindi chote cha maandalizi na kujadiliwa kwa Bajeti hii, chini ya uangalizi wa kiongozi mahiri na mchapakazi Katibu Mkuu Khamis Mussa Omar. Shukurani hizi vile vile ziwafikie Viongozi na Watendaji wa Wizara zote za Serikali kwa maandalizi ya Hotuba za Bajeti zao na kwa kufanya kazi ngumu ya kuwasaidia Mawaziri wao kujibu hoja mbali mbali za Wajumbe wa Baraza hili, ambazo ni nzito na zinahitaji umahiri kuzipatia majibu sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi punde Mhe. Waziri amewasilisha Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali ya jumla ya Shilingi 444,638,206,000/- ili Wajumbe wako waujadili na hatimaye kuupitisha. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni mfupi lakini ni muhimu sana kwa ustawi wa

Wazanzibari, na ndio unaofanya kuwepo kwetu hapa tangu tarehe 09 Juni, 2010 kuwe na maana. Mswada huu tutakapoupitisha na kutiwa saini na Mhe. Rais utakaokuwa Sheria ambayo itatoa uhalali wa utekelezaji wa Bajeti tuliyoipitisha katika ukusanyaji wa mapato na kufanya matumizi ya fedha zitakazokusanywa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu lilipitisha Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa na Mhe. Waziri mwenyewe na kwa kuwa Baraza hili pia limepitisha mafungu ya Wizara moja moja, bila shaka hakuna sababu ya msingi itakayohalalisha kupingwa kwa mswada huu ambao ni njia tu ya kisheria ya kuhalalisha kile tulichokipitisha kwa umoja wetu. Kwa mantiki hiyo basi, napenda kutamka kwa niaba ya Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Baraza kwamba naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kuhusu mswada huo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono huko kuna jambo dogo ambalo tumeliona na tunadhani ni kasoro katika mswada huu. Mswada huu unajulikana kwa jina la **Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Shilingi 444,638,206,000/-** kama ulivyoandikwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la tarehe 24 Juni, 2010. Katika maelezo hayo neno '**mapato'** linakosekana. Hivyo, Kamati yetu inadhani hii ni kasoro kwani mapato ni sehemu muhimu ya Bajeti. Bila ya mapato hakuna matumizi. Mantiki ya pili ya upungufu niliouleza inatokana na ukweli kwamba, makisio ya karibu mafungu yote tuliyoyapitisha yana sehemu mbili - mapato na matumizi; sio matumizi pekee. Hivyo basi, sehemu hizo mbili ni muhimu zijitokeze kwenye maelezo ya jina *(title)* ya mswada huu. Kwa hivyo, jina la mswada huu ni vyema lingesomeka **Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mapato na Matumizi ya Shilingi 444,638,206,000/-** na kuendelea kama linavyosomeka katika mswada huo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi napenda kukushukuru kwa kunivumilia na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Wenyeviti wote na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu wa Taala* kwa kutufikisha salama katika hatua ya Mkutano huu wa Bajeti. Ninakushukuru nawe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu kutia baraka kidogo katika Mswada huu wa Makisio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaoishia Juni, 2011.

Mhe. Mwenyekiti, mantiki ya mswada huu ni kukamilisha kifungu cha 105 na 106 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuhusiana na masharti ya fedha yahusuyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambayo Kambi ya Upinzani kimsingi inakubaliana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha pili cha mswada huu nashauri baada ya maneno Idara ya Hazina paongezwe kiunganishi cha lugha ili sentensi iliyoko katika mstari wa kwanza iwe na maana kamili.

Katika kifungu cha tatu cha mswada huu, naomba kupata ufafanuzi juu ya maneno yalioko mstari wa kwanza – Kiasi ya fedha kilichotolewa au kiasi ya fedha kitachotolewa. Nini uhalisia.

Katika kifungu cha 4 (3) cha mswada huu, naomba kupata ufaufanuzi pia juu ya maneno yalioko mstari wa kwanza – fedha zozote zilizokopwa au fedha zozote zitazokopwa. Naomba uhalisia.

Katika kifungu cha sita kuna tafauti ya maana baina ya maelezo yalioko kwenye mswada huu wa Kiswahili na yale maelezo yalioko kwenye tafsiri ya Kiingereza, wakati maelezo ya mswada wa Kiswahili yanazungumzia fedha zinazohitajika kama malipo ya riba tu, yale maelezo yalioko kwenye mswada wa Kiingereza yanazungumzia mambo mawili *"Sum Required for Public Loan Redemption and Repayments of Interest"*. Je, naomba kuelezwa nini uhalisia, ni riba tu au ni riba pamoja na *Public Loan Redemption?* Naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kimsingi inakubaliana na mswada huu wa makisio, ila inaomba kukumbusha kwanza katika vifungu vya matumizi na mapato ya Wizara na Taasisi zake katika bajeti ya mwaka huu, Kambi yangu ya Upinzani haikukubaliana na matumizi katika ofisi ya vitambulisho tu. Naiomba Serikali kuzingatia maoni ya Kambi yangu juu ya utendaji kazi wa ofisi hiyo, ili marekebisho yapatikane kwa mipango ya Bajeti inayokuja.

Mhe. Mwenyekiti, pili Kambi yangu ya Upinzani kwa sauti kubwa imekuwa ikionesha wasi wasi juu ya Mipango ya Kibajeti juu ya suala zima la zao la karafuu. Hili ni jambo ambalo Serikali nalo halina budi kulifikiria na kulitafutia ufumbuzi kwa Mipango ya Kibajeti inayokuja.

Mhe. Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inakubaliana na Mswada huu wa Makisio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaoishia Juni, 2011 na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ninaunga mkono hoja ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Mapato na Matumizi ya Shilingi 444,638,206,000/- kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa kawaida hoja hii huwa haijadiliwi lakini kama kuna wajumbe wanataka kusema chochote kwa muda mfupi sana ipo nafasi hiyo imetolewa kwa mujibu wa Kanuni ya Baraza. Inaelekea Waheshimiwa Wajumbe wote wameridhika.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kufanya majumuisho baada ya uwasilishaji wangu na kufuatia kwa maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo leo yametolewa na Kaimu Mwenyekiti Mhe. Ali Suleiman Ali, ambaye pia ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti. Kwa hiyo, tunamshukuru sana.

Halikadhalika, naomba nimshukuru sana rafiki yangu Waziri Kivuli Mhe. Said Ali Mbarouk kwa mimi siku zote mwenyewe huwa anaona namtania lakini namwambia ukweli, mimi namwita *Chief Analyst*. Maana yake *Chief Analyst* ni mchambuzi mzuri sana. Kwa hiyo, yeye anaona namtania lakini huwa namwambia ukweli kabisa. Unajua wakati mwengine unapozungumza ukweli mtu anaona utani, lakini ni kweli kabisa Mhe. Said hata kwenye kamati tunamsifu sana kwa uchambuzi wake. Mhe. Said Ali Mbarouk nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kweli lazima nikiri kulikuwa na *typographical error* ndogo ndogo za hapa na pale ambazo ilibidi tuziwasilishe. Sasa hizo ilibidi tuziwasilishe pamoja na mswada wenyewe. Hizo nakuahidi tutaupitia kwa undani kabisa tuweze hapo baadae kutoa *fair copy* ya mswada wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze na Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, Mhe. Ali Suleiman Ali tunakushukuru sana kwa uchambuzi wako na sifa zote ulizozitoa kama nilivyosema jana kwa niaba ya Wizara tunazipokea. Mimi sifa hizi nirudishe kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu bila ya mashirikiano yenu, bila ya maswali yenu, bila ya kutupa kidogo mchakato mchakato, nafikiri na sisi tusingekuwa *attentive* kufanya kazi vizuri zaidi. Kwa hiyo, mimi nakushukuruni sana na tuendelee na moyo huo wa ushirikiano kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamo Mwenyekiti alitoa pendekezo katika jina la mswada liongezwe neno mapato iwe ‘mapato na matumizi’. Kwa kweli hilo ni *omission* kubwa sana na nikiri Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na yeye mheshimiwa na tutaliongeza hilo katika ile *final version* yetu ya mswada. Kweli kwanza tukusanye halafu tutumie. Kwa hiyo, ushauri wake kwamba

kwenye kichwa hichi cha maneno hili neno mapato liongezwe. Nakubaliana na yeye hilo tutalishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali yeye hakuwa na zaidi pale kulikuwa na kosa dogo tu ni laki mbili sio mia mbili. Tunashukuru aliposoma yeye aliirekebisha pia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri Kivuli kwenye kifungu cha pili tuongeze neno 'ya' baina ya Idara ya Hazina na Wizara ya Fedha. Nafikiri tukiongeza hivyo tutasoma kwa mtiririko mzuri sana.

Kifungu cha tatu lugha iliyopo ni sawa kwani kinafanya kazi baada tu ya fedha kutolewa kutoka Mfuko Mkuu. Yaani baada ya fedha kutolewa Mfuko Mkuu ndio hichi kifungu kinafanya kazi. Kwa hiyo, nafikiri lugha iliyopo kwa wenyewe wataalam wanasema ni sawa.

Mhe. Mwenyekiti, zamani mimi siku zote huwa namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu, sisi tunapochangia miswada hii ya kisheria anasema kuna lugha ya kisheria. Sasa sisi tukiongea ile lugha ya kawaida anasema aaa kuna lugha ya kisheria. Kwa hiyo, wanasheria wametushauri kwamba hii ije baada ya fedha kutolewa kutoka Mfuko Mkuu. Ndio maana tunasema kilichotolewa chini ya kifungu cha pili.

Kifungu cha nne tayari imerekebishwa 'zilizopewa'. Hiyo nafikiri hapo kweli kulikuwa na kosa tumeshalirekebisha. Mheshimiwa tunakushukuru sana.

Kifungu cha sita ni kweli na ukisoma tafsiri ya Kiingereza inasema *Redemption and Payment of Interest.* Lakini hata kwenye Kiswahili Mhe. Said Ali Mbarouk ni Marejesho ya Mkopo na Riba *(Payment of Redemption and Interest).* Kwa hiyo, nafikiri ni sawa. Hata ndani pia inaonesha malipo ya mkopo na riba. Kama mikopo imekuwa *missed* yaani tumeruka basi naomba tuongeze 'kama malipo ya mkopo na riba'.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nafikiri Mhe. Said Ali Mbarouk atakubaliana na mimi kwamba mara nyingi tafsiri ya haraka haraka kutoka Kiingereza kuja Kiswahili huwa kidogo hatuipati kwa asilimia mia moja kama hasa inavyokusudiwa. Lakini tutakaa chini tutatulia na wanasheria wetu tutaiweka sawa ili iweze kukidhi haja yake. Tunakubali Mhe. Said hilo tutalirekebisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk zaidi alizungumza kuhusu kadi za utambulisho. Wakati wa majadiliano ya bajeti ile ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ maoni mliyoyatoa kama serikali tumeyasikia na tumesema tutayafanyia kazi kwa kushirikiana pamoja. Maana yake hata mwanzo ile

concept yenyewe ya vitambulisho ilikuwa kidogo wengi hatuifahamu, tulikuwa tunaona labda ni kuijengea uwezo tu Chama Tawala. Lakini baadae wote tumekuja kukubaliana kwamba kweli kuna haja ya vitambulisho. Azma ya serikali kwamba kila mtu apate kadi ya utambulisho lakini kwa masharti yaliyopo, hili ndio suala la msingi.

Hawezi leo Mhe. Said Ali Mbarouk mtu anayekaa Gando aje kwangu Tomondo ahamie pale aseme nimpe kadi ya utambulisho kwa kupiga kura hivyo haitowezekana. Kwa hiyo, tujitahidi tufuate taratibu ziliopo. Sasa hayo ndio mambo ya msingi ambayo Afisi yetu ya Vitambulisho inayafuata na kwa kweli inajitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano wakati wa uandikishaji nilikutana na sahibu yangu mkubwa Mhe. Zahra Ali Hamad kule anatetea watu wake na mimi nawatetea watu wangu. Lakini kwa pamoja tukakubaliana kwamba kweli la msingi wa pale wakubalike wa pale. Maana yake alinikuta mimi moto mkali kweli kweli, akaniambia tulia Mhe. Waziri, watu wangu walio hapa basi tuwakubalie, kwa hivyo tuwape fursa wenyewe watu wa vitambulisho wafanye kazi zao kwa mujibu wa taratibu zao.

Mhe. Mwenyekiti, sisi serikali tunataka kila mmoja wetu apate kadi ya utambulisho kwa mujibu wa taratibu ziliopo na kwa mujibu wa anapoishi. Hili halina mjadala, tunasema kila mtu apate. Vile vile Mhe. Rais wa Zanzibar suala hili amelisemea sana na amewahimiza. Ninachoomba sana sisi kama viongozi tuwaelimishe watu, ili wafuate hizi taratibu. Kwa hivyo, maoni yale mliotoa Mhe. Said tumeyasikia kama serikali tutayafanyia kazi.

Kuhusu suala la uimarishaji wa karafuu. Hili nalo tumelisikia kwanza kwenye uzalishaji huko tushirikiane. Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira nafikiri alitolea ufafanuzi wakati wa bajeti yake, hata sisi jana tulizungumza kwamba bado tutaendelea kuliimarisha zao la karafuu. Lakini tunachoomba tusaidiane kama Waheshimiwa Wawakilishi, tusiyawache mashamba yakaharibika mpaka wakati wa mavuno tu.

Pia kwenye magendo ya karafuu, tusaidiane sana kwamba hilo zao kidogo lililopatikana basi liuzwe kwenye njia ya halali na sisi kama serikali tutajaribu ku- facilitate ili kuona labda matarajio yetu ya usoni ile marketing system kama tutaweza kuja kuibadilisha huko mbele. Naomba sana tufahamike kuwa sio kama serikali imedharau zao hili bado tutaendelea kuliimarisha na ubora wa zao letu la karafuu, ndio kitu kikubwa sana na haiba yetu na hata hao Indonesia na Brazilian bado hawajaupata ubora wa karafuu zetu. Kwa hivyo tuna kila njia na kila sababu ya kujivunia zao letu na juhudi zetu. Kwa hivyo, naomba

tushirikiane ili tuliimarishe kweli kweli, tuyaimarishe mashamba yetu, tuzivune na tuzianike.

Mhe. Mwenyekiti, unajua kwa sababu sisi hatu *determine* bei, lakini tukiwa na karafuu nyingi basi hao wanaozalisha wengine huko tunaweza tukawa *overshadow* kwenye uzalishaji, kwa sababu *quality* yetu ni nzuri sana. Kwa hivyo, napenda kumuhakikishia Mhe. Said kwamba suala hili serikali hatulidharau, maoni yote mliotoa kambi ya upinzani na hata upande wa chama tawala tumeyasikia na tutayafanyia kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya maelezo machache naomba sasa nimalizie kwa kusema kwamba yote tumeyakubali na tutayafanyia kazi katika marekebisho ya mswada wetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima, ili liweze kuupitia mswada wangu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nne na Arubaini na Nne, Mia Sita na Thelathini na Nane Milioni, Mia Mbili na Sita Elfu Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, kwa mwaka wa Fedha unaoishia Siku ya Tarehe 30 Juni 2011 na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo yanayohusiana na hayo

Kifungu cha Kwanza Jina Fupi

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijachangia, lakini nadhani kwa kuweka Hansard vizuri bora niseme chochote. Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti alipokuwa akitoa maoni ya kambi yao, alipendekeza jina fupi la kutumika. Lakini mimi sikubaliani nalo. Hii ni *appropriation bill* ni tofauti na makadirio na matumizi, hii sio makadirio na matumizi. Humu kinachoelezwa ni idhini ya kutumia fedha ambazo tayari zimeshakuwa *connected*. Sasa nadhani tukisema kwamba ni mswada wa mapato na matumizi itakuwa ni *wrong*, *appropriation* haina uhusiano wowote na mapato. Nilikuwa nasahihisha tu, kwa hivyo nafikiri ungebakia vile vile Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Inaonekana imekubaliwa hoja yako Mhe. Haji Faki Shaali. Kwa hivyo kifungu hiki cha kwanza kinakubaliwa.

Kifungu cha Pili	Utoaji wa shilingi mia nne na arubaini na nne bilioni, mia sita thelathini na nane milioni, laki mbili na elfu sita kutoka mfuko mkuu wa hazina wa serikali.

Mhe. Haji Faki Shaali: na hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, naomba nisaidie. Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo komyuta imeruka kwenye hii ya Kiingereza. Kwa hivyo, nilikuwa ninamsaidia Mhe. Waziri tu, kuwa ukiiangalia huu mswada wa Kiingereza kwenye *registration and identity card office* pale pana *blank* hazikutiwa fedha zake. Lakini katika Kiswahili zimewekwa. Kwa hivyo, katika ule mswada wa Kiingereza kompyuta imeruka, hivyo naomba vile vile usahihishe.

Mhe. Mwenyekiti: Haya kifungu cha pili kinakubaliwa.

Kifungu cha Tatu	Makisio ya Fedha zilizokubalika.
Kifungu cha Nne	Uwezo wa waziri kukopa.
Kifungu cha Tano	Uwezo wa waziri wa maombi ya ziada.
Kifungu cha Sita	Marejesho ya mikopo na riba pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha Saba	Kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo.
Kifungu cha Nane	Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu, kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mwada wa Sheria wa Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na (MBLM) anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali, kwa Mwaka 2010/2011 usomwe mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, ameshatoa hoja. Sasa niwahoji tena kwa mara nyengine Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nne na Arubaini na Nne, Mia Sita na Thelathini na Nane Milioni, Mia Mbili na Sita Elfu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2011, na Kuhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Sasa umepitishwa Rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote tulizokusudia katika Baraza hili la Saba sasa zimekamilika. *(Makofi).*

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa mashirikiano yaliyopelekea kikao hiki kumalizika vizuri sana. Sasa hapa nina tangazo moja. Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu, mnatangaziwa kwamba Mhe. Shamsi Vuai Nahodha ambaye ni Waziri Kiongozi wa Zanzibar anawaalika wajumbe wote wa Baraza hili kuhudhuria katika ghafla fupi, hapa imeandikwa *Cocktail Party* itakayofanyika leo Alhamis tarehe 15/07/2010 saa 1:30 barabara hapa katika viwanja vya Baraza la Wawakilishi. Wajumbe wote mnaombwa sana kuhudhuria katika ghafla hii.

Sasa niwashukuruni tena kwa mara nyengine, na niombe basi kuahirisha kikao hiki cha Baraza mpaka hapo kesho tarehe 16/07/2010 siku ya Ijumaa saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 3:40 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 16/07/2010 saa 3:00 za asubuhi)